

DC Kondoa ajitosa sakata la Sikika

NA KHAMIS MKOTYA

MKUU wa Wilaya ya Kondo, Omar Kwaangw', amekosoa uamuzi wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kondo wa kulifukuza Shirika la Sikika wilayani hapa.

Akizungumza na MTANZANIA ofisini kwake juzi, Kwaangw', alipingana na uamuzi huo uliofanywa Julai 26, mwaka huu na kueleza kuwa busara haikutumika katika suala hilo.

Alisema uamuzi huo hauna afya kwa maendeleo ya Kondo kwa kuwa unaweza

kuvunja moyo kwa mashirika mengine yakashindwa kufanya kazi na halmashauri hiyo kwa hofu ya 'kunyongwa'.

"Shirika hili linafanya kazi ya kujenga uwezo wa wananchi na kukuza uwajibikaji. Katika timu ya SAM walifanya kazi vizuri pamoja kwa kushirikiana na madiwani, wadau wengine na wananchi.

"Ripoti ya kwanza ilipotoka ilionyesha udhaifu katika sekta ya afya, madiwani walipinga ripoti wakasema taarifa ile si sahihi. Hapo ndipo uhusiano wao ulipoanza kutetereka.

"Walikaa wakajadiliana wakarekebishana wakaendelea na kazi. Awamu ya pili ya ufuatiliaji madai ya madiwani kutukanwa na shirika yalijitokeza mgogoro ukaibuka tena.

"Kutokana na madai hayo, ni wazi kuwa shirika kama taasisi haliwezi kutukana. Tulitarajia kwamba kama kuna mtu aliyetukana aondolewe kazi iendelee badala ya kulifukuza shirika," alisema Kwaangw'.

Alisema uamuzi uliofikiwa na madiwani ulikuwa na chembechembe za msukumo hasa kutokana na kushikilia

msimamo wao licha ya kushauriwa na wadau wengine kutumia busara katika jambo hilo.

Akizungumzia hatima ya suala hilo, alisema kulingana na taratibu hana mamlaka ya kuingilia uamuzi wa Baraza la Madiwani na suala hilo linafanyiwa kazi na mamlaka za juu.

"Tangu jambo hili litokee tumeona na kusoma katika vyombo vya habari watu mbalimbali wamepinga uamuzi huu pia tumeona mashirika mengine yamelaani na kusema kuwa baraza la madiwani limekiuka katiba.